**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**
**MTIHANI WA MOKO KATA YA MFARANYAKI 2024**
**SOMO LA MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI DARASA LA VII**

## SEHEMU A:
## Chagua herufi ya jibu sahihi

1. i) Ni tukio gani la kihistoria tunalikumbuka ifikapo tarehe 26 Aprili kila mwaka?
   a) siku ya uhuru  b) Kifo cha Mwalimu Julius K. Nyerere
   c) Muungano wa Tanganyika na Zanzibar  d) Mapinduzi ya Zanzibar
   e) Kifo cha Edward Moringe Sokoine

   ii) Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kuwa nchi moja inayoitwa __________
   a) CCM  b) Tanzania  c) TAZAMA  d) Uhuru wa Tanganyika  e) Tanzanaiti

   iii) Ipi kati ya nchi zifuatazo ilipata uhuru kwa njia ya vita?
   a) Ghana  b) Tanganyika  c) Msumbuji  d) Zambia  e) Uganda

   iv) Ukame huathiri______ katika shughuli za uzalishaji mali
   a) Wakulima na wavuvi  b) Wakulima na wafugaji  c) Wafanyakazi viwandani
   d) Mafundi ujenzi  e) Wafanyakazi maofisini

   v) Vifuatavyo ni vyama vya siasa vilivyopigia uhuru wa Afrika chama kipi kilipelekea uhuru wa ANGOLA__________ a) MPLA  b) FNLA  c) UNITA  d) UNIP  e) TANU

   vi) Haigrometa ni kifaa kinachotumika kupima_________
   a) Unyevu  b) Jotoridi  c) Mvua  d) Mwanga  e) Upepo

   vii) Latitudo, mwinuko na umbali kutoka bahari ni mambo muhimu yanayoathiri______
   a) Tabia ya nchi  b) Mfumo wa jua  c) Hali ya hewa  d) Mikondo ya bahari
   e) Upepo

   viii) Wajerumani walitawala Tanganyika baada ya tukio gani?______
   a) Vita vya kwanza vya dunia  b) Mkutano wa Berlin  c) Vita vya pili vya Dunia
   d) Kukomesha biashara ya watumwa  e) Kenya kupata uhuru

   ix) Kivuli chepesi ambacho kinatokea wakati wa kupatwa kwa jua kinaitwa____
   a) Umbra  b) Obiti  c) Penumbra  d) Mizazi  e) Mzazi

   x) Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo husababisha _______
   a) Mifugo kunenepa  b) Wachunga kuchoka  c) Mmonyoko wa udongo
   d) Majani kuongezeka  e) Tsunami

   xi) ____ ni sehemu katika Tanzania ilipovumbuliwa fuvu la binadamu wa kale.
   a) Isimila (Iringa)  b) Kondoa (Dodoma)  c) Kaole (Pwani)  d) Bonde la Olduvai (Arusha)
   e) Engaruka (Arusha)

   xii) Lifuatalo ni shirika la kimataifa linalohusika na kushughulikia wakimbizi________
   a) UNHCR  b) UNICEF  c) ILO  d) WHO  e) FAO

   xiii) Kwanini wanafunzi wanashauriwa kutovaa viatu vyenye visigino virefu?
   a) Wataumwa matumbo  b) Husababisha wawe warefu  c) Husababisha maumivu ya misuli
   d) Husababisha mwili kuchoka  e) Husababisha kichwa kuuma

   xiv) Kuna umuhimu gani wa kukausha chungu baada ya kufinyanga?___
   a) Kukifanya kiwe imara  b) kukifanya kiwe na rangi  c) Ili kuweza kukiweka nakshi
   d) Kukifanya kiwe chepesi  e) Kukifanya kiwe chungu

   xv) Mahitaji muhimu mawili yanayotakiwa wakati wa hedhi ni______ na ______
   a) Sketi na sado  b) kanga na sketi  c) sodo na chupi  d) kitenge na kanga  e) kitenge na chupi

2. **Oanisha kifungu A na Kifungu B ili kupata herufi ya jibu sahihi**

| **KIFUNGU A** | **KIFUNGU B** |
|---|---|
| i) Kipimio cha unyevuanga<br>ii) Afelioni<br>iii) Emil von zelewski<br>iv) 1939 – 1945<br>v) Makao makuu ya umoja wa Afrika (AU) | A. Barometa<br>B. Kamanda wa ujerumani alieuwawa na majeshi ya Mkwawa<br>C. Vita vya kwanza vya dunia<br>D. Dunia kuwa mbali na jua<br>E. Arusha (Tanzania)<br>F. Vita vya pili vya dunia<br>G. Haigrometa<br>H. Dunia kuwa karibu na jua<br>I. Kamanda wa kikatili wa kijerumani<br>J. Adis Ababa (Ethiopia) |


## SEHEMU B:

### Jaza nafasi zilizoachwa wazi

3. i) Eleza kwanini maeneo ya pwani ya bahari ya pasifiki huathiriwa na Tsunami_______
   ii) Taja nchi mbili za Afrika ambazo hazikutawaliwa na wakoloni a)__________ b)________
   iii) Orodhesha athari za ukataji wa miti katika mkoa wako a)__________ b)________
4. i) Ni mnyama gani wa kwanza kufugwa na binadamu __________
   ii) Taja vitangulizi vya wakoloni a)__________ b)________ c)____________
   iii) Taja vifaa vilivyotumika kutengeneza moto katika zama za mawe za kati a)________ b)________
5. i) Taja mila na desturi potofu (mbili) a)__________ b)________
   ii) Bomba la mafuta kutoka Tanzania hadi Zambia_______________
6. i) Tofautisha kati ya tabianchi na hali ya hewa_____________
   ii) Vita vya majimaji vilitokea mwaka gani?___________

## SEHEMU C: RAMANI

7. Tazama ramani iliyo hapa chini na utumie kujibu maswali i-v




i) Andika jina la ziwa lilioneshwa kwa herufi A_______________
ii) Andika jina la bahari iliyooneshwa kwa herufi D_________________
iii) Andika jina la ziwa lililooneshwa kwa herufi B___________________

iv) Andika jina la ziwa lilioneshwa kwa herufi C ____________________

v) Ni nini umuhimu wa ufunguo kwenye ramani hapo juu ___________